



س1: هل يجوز لبس الثوب الضيق الذي يبرز الظهر للمرأة والثديين والخصر، والذي يبرز محاسن المرأة، والذي يكشف الذراعين والرقبة وبعض من الصدر أمام النساء والمحارم، وهل يجوز لبس الثوب الضيق أمام النساء فقط من المحارم أو غيرهن من النساء الأجنبية المسلمات؟ ج1: هذا السؤال له شقان: الأول: في لباس المرأة للضيق الذي يصف أعضاءها، فيعلم من نصوص الشريعة وقواعدها أنه يشترط في لباس المرأة المسلمة أن يكون واسعاً فضفاضاً لا ضيقاً، وهذا هو الذي يوافق الغرض من اللباس، وهو: الستر، وحجب بدن المرأة عن نظر الأجانب منعاً للفتنة والفساد، واللباس الضيق ينافي هذه المقاصد الشرعية؛ لما فيه من إبراز حجم البدن وأعضائه، فلا يتحقق الغرض المراد من الستر، بل قد يكون أدعى للفتنة والافتتان. وعليه فيحرم على المرأة المسلمة أن تلبس اللباس الضيق أمام محارمها سوى زوجها، ويحرم عليها أمام نساءها إذا كان من السرة إلى الركبة كالبنطلون، أو كان لسائر بدنها لكن يحصل به فتنة النساء والإثارة. الشق الثاني من السؤال: فيما يحل لها إظهاره من زينتها أمام محارمها غير زوجها، فهو: وجهها، وكفها، وخلخالها، وقرطها، وأساورها، وقلادتها، ورأسها، وقدامها. المصدر: اللجنة الدائمة للبحوث العلمية والإفتاء

#### SWALI:

Je inafaa kuvaa **nguo yenye kubana** ambayo inadhahirisha mgongo wa mwanamke na matiti yake na kiuno chake. Na nguo ambayo inaonyesha uzuri wa mwanamke na inaonyesha dhira mbili za mkono na shingo yake na baadhi ya sehemu za kifua chake mbele ya wanawake wenzake na ndugu zake wa karibu. Na je inafaa kuvaa nguo yenye kubana mbele ya wanawake wenzake tu miongoni mwa wanawake ambao ni ndugu zake wa karibu na wanawake wengine wa kando (wasio ndugu zake) ?

#### JIBU

[[ Swali hili lina pande mbili: Upande wa kwanza; Kuhusu vazi la mwanamke lenye kubana ambalo linadhahirisha viungo vyake; Inafahamu kutokana na miongozo ya sheria ya Kiislamu na Misingi yake kwamba limewekwa **sharti katika nguo ya mwanamke** wa kiislamu iwe pana

**isiyobana** . Na sharti hili ndilo lenye kuafikiana na lengo la **mavaz** nalo ni **kujisitiri na kufunika mwili wa mwanamke dhidi ya kutazamwa na wanaume wa kando ili kuzuia fitina na uharibifu**. Na mavazi yenye kubana yanapingana na makusudio na malengo haya ya kisheria, kwa sababu katika uvaaji huo kuna kudhahirisha umbile la mwanamke na viungo vyake , hivyo lengo la kujisitiri likusudiwalo halifikwi; bali vazi hilo linaweza kuwa ni kichocheo kikubwa cha fitina. Kwa mujibu wa maelezo hayo; **ni haramu juu ya mwanamke wa kiislamu kuvaa vazi lenye kubana mbele ya ndugu zake wa karibu wa kiume, isipokuwa mumewe** . Na ni haramu juu ya mwanamke wa kiislamu kuvaa vazi lenye kubana **mbele ya wanawake wenzake** endapo litakuwa limefunika kuanzia katika kitovu mpaka katika magoti tu, kama vile suruali, au liwe limefunika maeneo mengine ya mwili lakini likawa linawafitinisha wanawake wenzake na kuchochea hisia zao.

Upande wa pili wa swali: Kuhusu kinachofaa kudhahirishwa miongoni mwa mapambo ya mwanamke mbele ya ndugu zake wa karibu wa kiume, kinyume na mume wake, nacho ni ; **uso wake na viganja vyake vya mikono, na vikuku vyake , harenzi zake , na bangili zake na cheni yake, na kichwa chake na miguu yake ( chini ya miguu yake).**..]]

وصلى الله على محمد وآله وصحبه وسلم